

# Kuhusika katika jamii yako

## Jinsi tunavyoweza kusaidia

Aprili 2011



scottish  
refugee  
council

Community - Swahili

Kuzoea maisha katika Uskoti inaweza kuwa ngumu lakini mashirika mengi, tunayofadhili, ambayo yamewekwa ili kusaidia.



### **Jinsi wafanyakazi wa kuhusika kwa jamii wanavyoweza kusaidia**

Timu yetu hutoa ushauri kwa watafuta kimbilio na wakimbizi wanaotaka kuanzisha mashirika yao ya uwakilishi. Sisi pia hutoa ushauri kwa jumuiya ya mitaa ambazo hutoa huduma kwa watafuta kimbilio na wakimbizi, au wanaoinua uaminifu katika jumuiya zao.

Sisi hufanya kazi ili kuhakikisha kuwa mashirika ya wakimbizi na wanachama wao wana sauti katik angazi zote katika jamii ya Waskoti.

Tunaweza kutoa maelezo kuhusu mashirika ya jumuiya ya wakimbizi na mifumo inayotoa huduma hizi, ushauri na maelezo kwa watafuta kimbilio na wakimbizi walio mitaani.

Tumejiunga na mawakala wengine na huduma ambazo hutoa usaidizi kwa mashirika ya jumuiya ya wakimbizi na tunaweza kukupendekeza kwao kwa usaidizi.

### **Mashirika ya Jamii ya Wakimbizi (RCOs)**

Wakimbizi wengi katika Uskoti wameanzisha mashirika yao ya jumuiya. Mashirika haya hutoa nafasi za kukutana na watu kutoka nyumbani mwao na kushirikiana kuhusu mazoea yao, matatizo na kupata suluhisho. Pia kuna vikundi vya wanawake-pekee, ambapo wanawake hukutana kushiriki kuhusu uzoefu wao na kutoa usaidizi kwa wanawake wengine walio na matatizo na masikitiko kama yao. Mashirika haya yanaweza kukusaidia kushirika katika jumuiya yako ya mtaa, kushiriki utamaduni wako na kutoa usaidizi.

### **Jua mengi zaidi**

Jua mengi zaidi, pamoja na maelezo ya mawasiliano ya RCO, kwenye tovuti yetu:

[http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/how we can help/i want to get involved in my community/refugee community organisations](http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/how_we_can_help/i_want_to_get_involved_in_my_community/refugee_community_organisations)

## **Mitandao ya Ujumuishaji**

Mitandao ya Ujumuishaji katika Glasgow ni vikundi vya mawakala wa mitaa, vikundi vya jamii na wafanyakazi wasio wa kulipwa wanaopanga na kutoa huduma kwa watafuta kimbilio na Wakimbizi katika eneo lao. Huduma hizi zinaweza kuwa pamoja na maelezo na ushauri, madarasa ya Kiingereza, huduma za uwasilishaji, mambo ya watoto na watu wazima, pamoja na huduma na matendo ya wanawake –pekee, mipango ya kitamaduni, na usaidizi wa kiakili na wa utendaji.

## **Jua mengi zaidi**

Jua mengi zaidi, pamoja na tondoti zaidi za mawasiliano za Mifumo ya Usimamizi, kwenye tovuti yetu:

[http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/how\\_we\\_can\\_help/i\\_want\\_to\\_get\\_involved\\_in\\_my\\_community/integration\\_networks](http://www.scottishrefugeecouncil.org.uk/how_we_can_help/i_want_to_get_involved_in_my_community/integration_networks)

## **Jinsi ya kuwasiliana na wafanyakazi wetu wa Mipango ya Jamii**

Unaweza kuwasiliana nasi katika [cdenquires@scottishrefugeecouncil.org.uk](mailto:cdenquires@scottishrefugeecouncil.org.uk) au upige simu kwa 0141 248 9799 ili kuongea na mmoja wa memba wa timu. Sisi ni timu ndogo iliyo na uwezo mdogo, kwa hivyo tunaweza kutowasiliana nawe mara moja kuhusu tatizo lako. Hata hivyo, tutajaribu kuwasiliana nawe haraka iwezekanavyo.